Wasimamizi wa kampuni waliitikia majukumu haya kwa kuanzisha hatua kadha, miongoni mwao ikiwa ni kuchukua hatua za kuthibiti gharama, na kuimarisha ujuzi kwa kuweka mitambo mipya ya kazi na kila mara kuhusisha mashirika mbali mbali ya serikali kukabiliana na kuingizwa kimagendo kwa bidhaa bandia katika soko.

Uuzaji wa bidhaa zetu mwaka wa 2007 ulileta pato la shilingi bilioni 2.3 na faida kabla kutozwa kodi ya shilingi milioni 179 ikilinganishwa na pato la shilingi bilioni 2 na faida ya shilingi milioni 234 mwaka uliotangulia.

Kupungua kwa bei ya zinki na kuimarika kwa sarafu ya hapa nchini kunatarajiwa kupunguza gharama yetu ya ununuzi wa mali ghafi mwaka wa 2008. Kampuni itaendelea kuzingatia uthibiti wa gharama na kuimarisha ujuzi wa utendaji kazi, na vile vile kushughulikia kwa maakini uuzaji bidhaa zetu katika soko la nje na kuongeza aina mbali mbali ya bidhaa ili kuhakikisha ukuaji na mapato bora kwa wenye hisa wetu.

### Uuzaji na Masoko:

Mnamo mwaka wa 2007, tulishuhudia ongezeko la bidhaa zetu aina ya Energizer na Tochi katika masoko ya hapa nyumbani na nje. Viwango vya uuzaji katika soko la hapa Kenya viliongezeka kwa asilimia 28 mwaka uliotangulia, ilhali katika soko la nje viliongezeka kwa asilimia 508 kwa bidhaa aina ya Energizer. Uuzaji wa bidhaa za Tochi uliongezeka kwa asilimia 13 mwaka wa 2006.

Kulikuwa na ongezeko la asilimia 2 kwa viwango vya uuzaji betri aina ya 'D' katika soko la hapa nyumbani, ikilinganishwa na viwango vya mwaka uliopita. Uuzaji betri aina ya 'D' katika soko la nje uliongezeka kwa asilimia 5 mwaka wa 2007. Hata hivyo tumeshuhudia hali ya wateja kubadili chaguo la bidhaa wapendazo na kununua bidhaa za bei nafuu hasa betri za rangi ya samawati yaani (Blue) aina ya 'D'(950) zilizo na bei nafuu ambazo mauzo yake uliongezeka kwa asilimia 17 ikilinganishwa na viwango vya uuzaji vya mwaka 2006. Tulipata hasara ya kiwango cha asilimia 10 kwa betri za rangi nyekundu aina ya 'D' (1050), na za rangi nyeusi aina ya 'D' (1250). Tunashuku kwamba baadhi ya washindani wetu wamepunguza bei za bidhaa zao, na kufuatia matamshi ya Halmashauri ya Ukusanyaji Ushuru nchini KRA, hawajalipa ushuru wa kuleta bidhaa kutoka nje. Tunaendelea kuchunguza hali hizi na kutoa habari muhimu kwa idara za serikali zinazohusika, tukitumai kwamba hatua kali zitachukuliwa kuhusu swala hili.

Tunaendelea kushuhudia ongezeko kubwa katika uuzaji wa bidhaa zetu za alkaline na kadiri bidhaa zetu zinavyoendelea kuwa za kiasi kidogo, tutaendelea kuwapa wateja wetu bidhaa zitakazotosheleza mahitaji yao, kama vile betri za kiwango cha AAA.

Tuna bidhaa ya kufurahisha ya betri aina ya 'Energizer Lithium' na tutaifanyia kampeini kubwa ya uuzaji mwaka wa 2008 kwa sababu, kweli ni betri inayodumu kwa muda mrefu sana Duniani ya kiwango cha AA. Shughuli za kutangaza bidhaa zetu katika vituo vyetu muhimu zitazingatia wateja wetu mwaka wa 2008. Hili ni wazo jipya na la kufurahisha linalopaswa kuimarisha maudhui yetu katika soko. Tunawekeza mali muhimu nyuma ya juhudi hizi na kwa wakati huu tuna maduka mawili ya Supermarket yaliyoanzishwa katika mtindo huu.

Tunapanua uwezo wetu wa utoaji bidhaa ndogo zenye nguvu ambazo ni pamoja na betri za kuweka chaji kwa soko la Kenya na kuna ahadi ya bidhaa zaidi za aina mbali mbali mwaka ujao.

**Ubora, Usalama, Afya na Mazingira:**

Katika kampuni ya Eveready, tunaamini kwamba wenzetu ni kiungo muhimu sana kwetu, na kwamba usalama na afya yao ni jukumu letu kubwa. Eveready imejitolea kutekeleza na kudumisha maongozi na mifumo inayowianisha malengo ya shughuli zake na mafanikio ya ulinzi wa kimazingira, afya na usalama wa wafanyakazi wake, wateja na jamii. Hivyo basi tunajitahidi kutimiza au kupita viwango vyote vya Kenya na vile vile, viwango vilivyowekwa na EBC. Kuhusiana na hayo, mafunzo hutolewa mara kwa mara na EBC na ukaguzi hufanywa ili kuthibitisha usimamizi wa miradi na kutambua nafasi zilizoko ili kuimarisha zaidi usalama na afya yetu.

Malengo yanayohusu ubora na mazingira yamekuwa yakizingatiwa katika mipango yote naalum ya usalama, afya na mazingira tangu kampuni ilipobuniwa. Tunazingatia viwango vya kudumisha matumizi ya kawi na mfumo mahsusi wa kuzingatia masharti ya kimazingira. Vile vile, tulidumisha mpango wetu wa uondoaji maji taka katika kiwanda chetu mwaka wa 2007. Hakuna maji yanayotumiwa katika mpango wetu wa utengenezaji bidhaa yanayoondolewa kiwandani. Maji hayo husafishwa na kutumiwa tena katika kiwanda hicho. Pia tunatumia mtindo huu kwa taka ngumu na kuhimiza kupunguza na kuzitumia tena taka zilizohuishwa. Tuna mpango imara wa kupunguza taka na kawi, unaotuwezesha kufikia kiwango cha upunguzaji taka cha asilimia 2.5 ikilinganishwa na mwaka 2006. Juhudi kabambe za mwaka 2007 zilisababisha kuhuishwa kwa maji taka ambayo hapo awali yalisafirishwa hadi katika eneo la taka la manispaa,

Tuliweza kupunguza majeruhi ya nje ya kazi kutoka majeruhi 28 mwaka 2006, hadi majeruhi 9 mwaka 2007 na kupunguza upotezaji siku za kazi kwa zaidi ya asilimia 50. Tunajivunia mafanikio haya na tunatazamia kuimarisha hali hii mwaka wa 2008.

Mnamo mwaka 2007. tulianza mpango wa kudumisha maendeleo unaohusisha upunguzaji kawi, matumizi ya maji, kupunguza taka, utoaji gesi ya viwandani na kuongeza matumizi ya kawi iliyotengenezwa upya. Tunatarajia kuwa mpango huu utaanza kutekelezwa mwaka wa 2008 kwa kupunguza athari hizi kwa asilimia 5 kila mwaka kama lengo letu.

**Wafanyakazi:**

Kuridhika kwa wafanyakazi ni muhimu kwetu. Kuwapa motisha, kuwasiliana nao na kuwatuza kwa upande mwingine, na vile vile kuhakikisha malipo yao ya baada ya kustaafu, masharti bora ya kazi, hali nzuri ya kufanyakazi kampunini inayounga mkono ushiriki wa wafanyakazi na kutoa nafasi za kujiendeleza kielimu na kuongeza mafunzo ni mambo ambayo sisi katika Eveready huyapa umuhimu maalum kuhusiana na wafanyakazi wetu. Tuna zaidi ya wafanyakazi 350 na mnamo mwaka wa 2007 tulitumia zaidi ya shilingi milioni 15 kuwapa mafunzo.

Mafunzo katika Eveready mwaka wa 2007 yaliandaliwa ili kuunga mkono malengo ya biashara yetu. Mafunzo haya yalihusisha masomo mbali mbali yakiwemo ya kiufundi, usimamizi, usalama, fedha, uuzaji na huduma ndogo ndogo miongoni mwa mambo mengine. Kampuni ya Eveready hutoa nafasi za mafunzo kwa wafanyakazi wakiwa kazini kwa viwango mbali mbali vya wafanyakazi wa ndani ya kampuni na wale wa maeneo ya EBC kote duniani. Mafunzo ya uzimamizi wa utendaji kazi yalifanywa mwaka huo na mafunzo haya yalishughulikia sehemu mbili za utendaji kazi wa kibinafsi, ni nini malengo ya kampuni, na ni jinsi gani ya kutimiza malengo haya kwa kuzingatia tabia na uwezo wa wafanyakazi kupitia mbinu ya kuregesha mawasiliano kwa kuzingatia mtindo wa "Simama, Anza na Endelea".

Tunaendelea kutoa mafunzo ya uuzaji kwa kundi letu la uuzaji na wagawaji wa bidhaa zetu. Mnamo mwaka 2007 tuliwapa mafunzo maafisa wetu katika ujuzi wa bidhaa, uuzaji, kutangaza na kuonyesha bidhaa. Mafunzo haya yalirahisishwa na Meneja wa Energizer wa eneo hili wa mafunzo na maendeleo wa EBC. Usalama ni muhimu sana kwetu na tunaendelea kudumisha viwango vya usalama na kuzingatia kikamilifu sheria za usalama za Kenya. Kuhusiana na haya, tuliwapa mafunzo wanachama wa kamati yetu ya usalama katika kuzingatia maswala muhimu ya wafanyakazi, huduma ya kwanza, matatizo ya kusikia, matatizo ya damu na shida za mawasiliano. Aina nyingine na mafunzo yaliyotolewa mwaka huo ni pamoja na mafunzo ya kifedha kwa mameneja wasiohusika na shughuli za kifedha na mafunzo ya kiufundi kama vile LOTO (lock-out tag-out), kujilinda, shughuli ndogo ndogo, vipengee vitano muhimu na kuendelea na mradi wa uboreshaji (CIP) unaopaswa kuboresha shughuli za kampuni.

**TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU**
**KWA MWAKA ULIOMALIZIKIA TAREHE 30, SEPTEMBA, 2007**

Tunaendelea kushirikiana na EBC katika kuimarisha utendaji kazi wa wafanyakazi wetu na kuhusiana na hili huwa tunatoa nafasi kwa wafanyakazi wetu kuzuru maeneo tanzu ya kampuni na kuhudhuria mikutano inayowapa wafanyakazi wetu nafasi na kujifahamisha na suluhisho za kimataifa katika nyanja zao mbali mbali duniani. Mnamo mwaka wa 2007, kulikuwa na ziara 15 zilizopangiwa wafanyakazi kusafiri katika eneo la Asia na Pacific kuhusiana na maswala yafuatayo:-Shughuli ndogo ndogo na Mradi wa Uboreshaji shughuli za kampuni CIP, Shughuli ndogo za Usimamizi; Uangalizi bora na Ubora wa Mifumo; Bidhaa na Shughuli za Ukarabati, Usalama, Afya na Mazingira(SHE); Shughuli za Utendaji kazi Kiwandani, Biashara ya Jadi (Uuzaji); Usimamizi wa aina za Bidhaa, Majina ya bidhaa na Huduma, Matangazo na Uhasibu muhimu (Uuzaji); Shughuli za Wafanyakazi na Huduma za kiufundi za Microsoft.

Tunatarajia kutumia shilingi milioni 15 katika juhudi zetu za mafunzo mwaka ujao. Pia tunatarajia ongezeko la gharama ya wafanyakazi katika mwaka wa 2008, kutokana na sheria mpya za wafanyakazi.

**Usimamizi wa Kampuni:**

Wakurugenzi wanaendelea kujitolea kudumisha viwango vya juu vya usimamizi wa kampuni wanavyoona kuwa ni muhimu katika kutekeleza majukumu yao ya usimamizi. Kama kampuni iliyoorodheshwa kwenye soko la hisa la Nairobi, tumejitolea kuhakikisha kwamba tumefikia na kuzingatia maongozi kuhusu taratibu za usimamizi wa kampuni za umma hapa nchini Kenya, yaliyobuniwa na Halmashauri ya Usimamizi wa Soko la Hisa ("CMA"). Tunatambua kwamba usimamizi bora wa kampuni ni muhimu katika usimamizi ufaao na tumebuni taarifa ya usimamizi wa kampuni inayomueleza kila mkurugenzi jukumu lake na uwezo wake, kazi zake, majukumu, wajibu na hasara.

Halmashauri inajitahidi kutoa maongozi, maono muhimu na uthibiti wa mazingira ili kutoa na kudumisha thamani ya huduma za kampuni kwa wenye hisa. Wanachama wote wa Halmashauri wana uwezo wa kufanya kazi zao na wanafahamu juu ya majukumu yao kwa wenye hisa wa kampuni. Halmashauri husaidiwa katika majukumu yake na kamati tatu muhimu ambazo ni:-

- Kamati ya Fedha na Hatari
- Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Pesa
- Kamati ya Marupurupu na Uteuzi

Kampuni inatilia maanani umuhimu wa mawasiliano na wenye hisa wake. Kampuni ya Eveready huchapisha taarifa zake za kifedha za kila mwaka na matokeo pia hupatikana kwenye tovuti ya mtandao wetu www.eveready.co.ke. Taarifa kamili ya shughuli za kampuni ya mwaka huo hupewa wanachama kila mwaka. Wanachama wote wana haki ya kuhudhuria mikutano mikuu ya kila mwaka ambayo ilani hutolewa siku 21 kabla ya mkutano. Kwenye mkutano mkuu wa kila mwaka, wenye hisa hupewa nafasi ya kuuliza maswali yoyote kuhusu maswala ya shughuli za kampuni.

Taarifa ya maongozi yetu kuhusu biashara na viwango vya tabia na sheria za ndani za biashara inasimamia uhusiano wetu na wakurugenzi wetu, wafanyakazi, wenye hisa, wagawaji bidhaa na jamii na ndio msingi wa thamani za kampuni yetu. Stakabadhi zaweza kupatikana kwenye tovuti ya mtandao wetu. Tunatuma kila mwaka kwa wagawaji wetu wote hapa nchini maongozi ya biashara yetu kwa washirika wa kibiashara na huwakagua wafanyakazi wetu kila mwaka kupitia fomu za maswali na majibu ili kuthibitisha kwamba tabia ya shughuli za biashara yetu ilitimiza maongozi ya kampuni ya Eveready katika mwaka uliopita. Tunaonelea kwamba maadili ya biashara katika viwango vyote vya kampuni yetu ni muhimu. Ikiwa tutapata tatizo la kimaadili litajadiliwa na kamati ya ukaguzi wa hesabu za pesa na halmashauri ikiwa ni pamoja na hatua tunazochukua kutatua hali yoyote ile. Panapostahili, tutatoa habari kwa idara za sheria ili mashtaka ya uhalifu yawasilishwe.

Tunajivunia kuwa mwanachama wa shirika la Umoja wa Mataifa la 'Global Compact.' Uanachama huu unatuhitaji kuwa na jukumu lisilo la kawaida: kufanya kazi yetu vyema, kwa kutegemewa na kiutaalamu katika vitengo vyote vya umma ambapo EEAL ina uhusiano mwema kwa wote wanaohusika.

**Jukumu la Kampuni kwa Jamii:**

Uraia bora wa kampuni na kuheshimu jamii tunayoihudumia ni muhimu katika kufanya biashara yetu hapa Kenya. Tumechunguza mwelekeo wetu wa jukumu la miradi ya kampuni kwa jamii ("CSR") kuwa na mtazamo bora na kama utaratibu ufaao tumebuni kamati ya CSR. Kamati hii iko katika usimamizi mkuu wa kampuni na hutoa mhadhara wa kushirikisha habari kuhusu juhudi za CSR na kustawisha shughuli bora kwa njia ya kuaminika. Tunanuia kuzingatia juhudi zetu za nia njema mwaka wa 2008 kuhusu miradi ambayo itashughulikia mahitaji ya kinamama na elimu na afya ya watoto. Mnamo mwaka 2007 michango kwa mashirika ya kujitolea na miradi ya jamii ilifikia jumla ya shilingi milioni 6. Hii inadhihirisha kujitolea kwetu katika kuibadili jamii tunayoihudumia. Ghasia ambazo zilifuatia mpango wa uchaguzi zilisababisha Wakenya wengi kuhama makazi yao. Waathiriwa wengi wa ghasia hizi walipata hifadhi huko Nakuru. Kampuni ya Eveready na wafanyakazi wake iliitikia mahitaji ya kibinadamu ya wakenya walioachwa bila makao kwa kuwapa msaada.

Kwetu sisi jukumu la kampuni kwa jamii CSR linapita kutoa na kuzingatia shughuli bora za kimazingira. Tumezingatia ongezeko la kawi na kupunguza athari za kimazingira kwa shughuli zetu na bidhaa. Tunajitahidi kusimamia taka zetu ipasavyo, kuthibiti gharama na kuwajibika. Hii inamaanisha kupunguza taka tunazoleta na vile vile kuongeza kiwango cha taka tunazohuisha.

**Sheria:**

Mwaka wa 2007 ulikuwa muhimu kwa kampuni ya Eveready. Eveready ina jumla ya kesi 22 zinazosubiri katika mahakama za hapa Kenya; kati yazo, 16 ziliwasilishwa dhidi ya kampuni ya Eveready huko Nakuru. Asilimia 59 ya kesi hizi ni madai ya malipo ya viwandani. Mahakama kuu na mahakama ya rufani katika kesi mbili za madai ya malipo ziliwasilishwa mwaka huo na kuamuliwa kwamba kampuni ya Eveready inaendesha mazingira salama na ya kiafya ya kazi na kwamba mafunzo ya kutosha yametolewa kwa wafanyakazi wote wa Eveready. Mahakama hizo zilipochunguza na kukadiria ushahidi uliowasilishwa zilikataa kuwapa malipo hayo walalamishi. Kwenye kesi hizo mbili, mahakama zilikataa kutoa shilingi milioni 5.6 kama hasara dhidi ya Eveaready na zikaweka hatua muhimu ya kisheria kwa kesi zijazo za aina hiyo. Tunatarajia kwamba uamuzi uliochukuliwa katika kesi hizi utadumishwa katika mwaka wa 2008 na kuendelea. Ningependa kukariri kwamba Eveready haitakubali ukiukaji wa viwango vya usalama, afya na mazingira ya utendaji kazi katika kiwanda chake na kwamba itaendelea kudumisha viwango vya juu vya maadili katika shughuli zake zote. Tutaendelea kukagua shughuli zetu ili kuhakikisha kwamba majukumu yetu yote kisheria yanatimizwa. Pia tutaendelea kufuatilia kesi hizi mahakamani panapokuwa na umuhimu na tumaamini kupata matokeo mema.

**Halmashauri ya Wakurugenzi:**

Kumekuwa na mabadiliko kadhaa muhimu katika Halmashauri. Mirabeau Da Gama Rose alijiuzulu katika Halmashauri mwaka wa 2007. Ningependa kumshukuru kwa mchango wake muhimu na wa kudumu aliotoa katika miaka aliyohudumu kwenye Halmashauri hii. Namkaribisha Bi. Susan Mudhune na Bwana Henry Kiplagat waliojiungana Halmashauri kama wakurugenzi wa kibinafsi wasiokuwa wafanyakazi mwaka wa 2007. Pia namkaribisha Bi. Fauzia Shah aliyechukua mahala pa Bwana Da Gama Rose kwenye Halmashauri. Ujuzi wao utakuwa wenye umuhimu mkubwa kwa kampuni. Bi. Mudhune na Bwana Kiplagat wamefikisha idadi ya wakurugenzi wetu kuwa 9.

**Mwisho:**

Ni maoni yetu kuwa hatua tulizochukua kusimamia gharama, kuboresha shughuli zetu za utengenezaji bidhaa na utendaji kazi ufaao na kuweka nguvu biashara yetu, zimebuni msingi thabiti kwa maendeleo zaidi. Soko letu linaendelea kuwa na ushindani mkali lakini kwa kuwa na aina mbali mbali ya bidhaa kuu na ahadi ya bidhaa mpya za kufurahisha, tutaimarisha nafasi yetu katika miaka ijayo. Tulishuhudia vurugu la kibiashara katika robo ya kwanza ya mwaka 2008 kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi zilizoikumba nchi hii kufuatia uchaguzi mkuu wa Desemba 2007. Hali hii iliathiri shughuli za biashara yetu katika baadhi ya sehemu za nchi hii hasa mikoa ya Magharibi, Nyanza na Rift Valley na tunatarajia kwamba hii itakuwa na madhara kwa biashara yetu katika mwaka wa 2008. Bei za mali ghafi huenda zikapanda na tunatarajia kuendelea kukumbwa na shinikizo la kupungua kwa bei za betri zetu katika soko. Haya ni majukumu na hatari zilizoko mbele yetu. Hata hivyo tutaendelea kuratibu shughuli zetu na kuimarisha utengenezaji bidhaa ili kulinda viwango vilivyoko vya utoaji bidhaa zetu. Tutaendelea na mikakati yetu ili kuimarisha thamani ya biashara yetu kuu, kuwasilisha bidhaa zinazoongeza thamani na vile vile kuzingatia athari za kimazingira. Tunaboresha betri zetu aina ya 'D' na tutazindua betri za kuweka chaji. Betri za kuweka chaji zinapaswa kupendwa na wateja kwa kuwa na gharama nafuu na rahisi kutumia.

Kwa niaba ya Halmashauri ya wakurugenzi na wasimamizi wa kampuni, nataka kukariri kujitolea kwetu kujenga kampuni kubwa inayozingatia kufikia viwango vikuu vya utendaji kazi na kujenga thamani ya wenye hisa. Pia ningependa kuwashukuru wenye hisa wetu, washirika wa kibiashara, wakurugenzi na wateja kwa msaada wao. Nawashukuru pia wafanyakazi kwa kujitolea kwao na bidii yao mwaka huo.

**Steven George Smith**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Tarehe 21, Januari, 2008:**

**Taarifa za Matarajio ya Siku za Usoni**

Baadhi ya taarifa kwenye taarifa hii zaeleza matarajio ya siku za usoni. Taarifa hizi zinahusu hatari na mambo yasiyoweza kubashirika ambayo huenda yakasababisha matokeo halisi kuwa tofauti na yale yaliyotajwa kwenye taarifa kama hizo. Ingawa kampuni inaamini kwamba matarajio yaliyoelezwa katika taarifa kama hizo ni ya maana, haiwezi kutoa hakikisho kwamba matarajio kama hayo yatathibitishwa kuwa sahihi. Maswala muhimu pamoja na mabadiliko katika hali ya kiuchumi kwa ujumla, kisiasa na kibiashara, vitendo vya washindani wa sasa na wanaoweza kuwa washindani, uwezo wa kuvutia wateja wapya na kudumisha wateja walioko na maswala mengine yanaweza kusababisha matokeo halisi kubadilika kutokana na matarajio ya kampuni na taarifa hizi za matarajio mema siku za usoni.

**BOARD OF DIRECTORS**
**FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER, 2007**

The biographies of the Directors holding office as at the date of this report are as follows:

**Naushad Merali - Board Chairman**

Mr. Merali is a businessman and the Chairman and Chief Executive Officer of the Sameer Group of Group of Companies. Sameer Group is a conglomerate of companies involved in telecommunications, energy, manufacturing, agriculture and finance sectors. Some of the companies in the group include Sameer Africa Limited (Formerly Firestone East Africa (1969) Limited), Sasini Tea & Coffee Limited, H Young & Company Limited, Equatorial Commercial Bank, Ryce Motors Limited, Kenya Data Networks and Swift Global Limited. Mr Merali has also served on various Presidential Committees relating to trade and social services. ***55***

**Steven George Smith - Managing Director**

Mr. Smith holds a Bachelor of Science degree in Industrial Technology from East Carolina University, Greenvile, North Carolina, USA. He has over 33 years experience in the EBC group starting as a production supervisor and rising through the ranks to a managerial position. He has worked with Eveready since 1998 as the Managing Director. ***57***

**Natarajan Radhakrishnan**

Mr Radhakrishnan represents Energizer in the Board of Eveready. He is currently the Finance director of Energizer Middle East and Africa Operations. He is a fellow Member of the Institute of Cost and Works Accountants of India and a member of the Institute of Company Secretaries of India. He has over 28 years senior managerial experience in various industries including financial institutions, manufacturing and service industries. He has been involved in Corporate re-structuring and several business development initiatives. With his extensive work experience in and exposure to the economies of the Middle East and various countries in the far East, Mr. Radhakrishnan is able to provide guidance and direction to Eveready's financial management. ***52***

**Akif H. Butt**

Mr Butt is a fellow of the Association of Chartered Certified Accountants (ACCA) and a Certified Public Accountant (CPA) and has over 25 years experience in financial management, corporate planning and strategic management. He initially trained and worked with PricewaterhouseCoopers in Kenya and the East African Region, Liberia and England. He joined the Sameer Group in 1989 and currently holds the position of Finance Director. He represents interests of the Sameer Group on the board of various companies. ***50***

**BOARD OF DIRECTORS**
**FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER, 2007**

**Peter Mwangi**

Mr Mwangi represents ICDCI as an alternate director on the boards of Kisii Bottlers Limited, Mount Kenya Bottlers Limited, Rift Valley Bottlers Limited, Eveready Batteries Limited, KWAL Holdings Limited and UAP Provincial Insurance Company Limited. Mr. Mwangi served as ICDCI's Company Secretary from 2000 to 2004 and was appointed Managing Director in December 2004 after serving in an acting capacity from August 2004. Mr. Mwangi is a member of ICPAK and the Institute of Certified Public Secretaries of Kenya (ICPSK). ***.38***

**Mr. Isaac B. Mogaka**

Mr. Mogaka represents Industrial & Commercial Development Corporation (ICDC) in the Board of Eveready East Africa Limited. He holds a Bachelor of Laws degree from the University of Nairobi. He is an Advocate of the High Court of Kenya having been admitted on 15th February 1982, a member of the Institute of Certified Public Secretaries (K) and an Associate Member of the Chartered Institute of Arbitrators. He is currently the Executive Director of ICDC. Prior to his appointment as the Executive Director on 19th June 2006, he served as the Corporation Secretary of ICDC for 12 years and as the Company Secretary of several ICDC subsidiary/Associate Companies. ***51***

**Susan Mudhune**

Ms. Mudhune holds a Bachelor of Arts Degree and an MBA from the University of Nairobi. She is a member of the Kenya Institute of Directors and the Chairman of the Kenya Commercial Bank Group (KCB). Prior to joining KCB, Susan worked in various management positions in the local banking industry for over 20 years. In addition, she serves as the national Chairman of the Kenya Girl Guides Association. In recognition of her outstanding achievements, the Kenya Institute of Bankers (KIB) awarded her Fellow of the Institute of Kenya Bankers in December 2003. ***58***



**Henry Kiptiony Kiplagat**

Mr. Kiplagat holds a Bachelor of Arts Degree and a Master of Arts in Education from the University of Lancaster, United Kingdom. Henry currently serves as the Chief Principal of the Moi High School, Kabarak and is also the Chairman of Moi Primary School Kabarak. Henry is a member of the Kabarak University Governing Council and a Trainer of trainers at the Kenya Education Staff Institute (KESI). Henry is a recipient of the Order of the Grand Warrior which was awarded to him by the Retired President Daniel Arap Moi in recognition of his service in the education sector in Kenya. ***41***

**Fauzia Shah**

Ms. Shah holds a Bachelor of Laws Degree and an advocate of the High Court of Kenya with over 20 years experiencee in corporate and commercial matters. Fauzia is also a Certified Public Secretary with over 15 years of company secretarial matters. She is currently employed by the Sameer Group as Company Secretary and In-house Counsel.

**EVEREADY EAST AFRICA LIMITED**

**SHAREHOLDING STRUCTURE**
**FOR THE YEAR ENDING 30 SEPTEMBER, 2007**

**Major Shareholders**

| Shareholder | No of Shares | % Holding |
|---|---|---|
| East Africa Batteries Limited | 73,754,377 | 35.12 |
| Industrial and Commercial Development Cooperation | 36,558,900 | 17.41 |
| Energizer International Inc. | 22,050,000 | 10.50 |
| Stanbic Nominees Kenya Ltd A/C ICDCI | 9,769,323 | 4.65 |
| CFCFS Nominees Ltd A/C 210 | 2,164,800 | 1.03 |
| Sebastian Mutimu | 610,900 | 0.29 |
| Johnson Mwangi Gitari | 325,300 | 0.15 |
| Amirali Husenalli Nathu | 275,000 | 0.13 |
| Mutimu Kang'atta and Company | 251,700 | 0.12 |
| Secumatt A/C Eveready | 250,400 | 0.12 |
| Others | 63,989,300 | 30.47 |
| **Total** | **210,000,000** | **100.00** |

**Distribution of Shareholders**

| Shareholding | No of Shareholders | Shares Held |
|---|---|---|
| No of Shares | | |
| Below 1000 | 140,167 | 32,286,869 |
| 1001-5000 | 7,128 | 14,212,286 |
| 5001-10000 | 653 | 4,645,932 |
| 10001-50000 | 379 | 7,210,298 |
| 50000-100000 | 38 | 2,619,715 |
| Above 100000 | 31 | 149,024,900 |
| **Total** | **148,396** | **210,000,000** |

***Based on the share register as at 30 November, 2007***

## CORPORATE INFORMATION
## FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2007

**DIRECTORS**
Mr. N. Merali - Chairman
Mr. S.G. Smith - Managing Director
Mr. A. H. Butt - Finance Director
Mr. M. Da Gama Rose (Resigned August 9, 2007)
Mr. N. Radhakrishnan
Industrial & Commercial Development Corporation (ICDC)
ICDC Investment Company Limited (ICDCI)
Ms. S. Mudhune (Appointed on March 22, 2007)
Mr. H. K. Kiplangat (Appointed on March 22, 2007)
Ms. F. B. Shah (Appointed August 9, 2007)

**AUDIT COMMITTEE**
Mr. P. Mwangi (representing ICDCI) - Chair
Ms. S. Mudhune
Mr. A. H. Butt

**REMUNERATION AND NOMINATION COMMITTEE**
Ms. S. Mudhune - Chair
Mr. I. Mogaka - (representing ICDC)
Ms. F. B. Shah

**FINANCE AND RISK COMMITTEE**
Mr. N. Radhakrishnan - Chair
Mr. I. Mogaka - (representing ICDC)
Mr. H. Kiplangat

**AUDITORS & TAX ADVISORS**
DCDM Associates
Certified Public Accountants
P. O. Box 10032-00100
**Nairobi**

**SHARE REGISTRARS**
Image Registrars Limited
Transnational House, Mama Ngina Street
P.O. Box 9287-00100
**Nairobi**

**ADVOCATES**
Kaplan & Stratton
Williamson House, Ngong Avenue
P.O. Box 40111-00100
**Nairobi**

**ADVOCATES**
Mukite Musangi & Company
Seguton Building, Kenyatta Avenue
P.O. Box 149-20100
**Nakuru**

**SECRETARY & COMPANY REGISTERED OFFICE**
Mr. I. A. Timamy
Standard Building, Wabera Street
TEL: 020-2216139
P.O. Box 44765-00100
**Nairobi**

**BANKERS**
Commercial Bank of Africa Limited
Barclays Bank of Kenya Limited
CITIBANK N.A

**EVEREADY EAST AFRICA LTD**

**DIRECTORS' REPORT**
**FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2007**

The Directors submit their report together with the audited financial statements for the year ended September 30, 2007, which disclose the state of affairs of the Company.

**PRINCIPAL ACTIVITIES**

The principal activities of the company are manufacturing and selling of Eveready dry cells "D" size batteries in East Africa and trading in an assortment of imported Eveready flashlights, batteries, razors and accessories.

**RESULTS AND DIVIDEND**

The net profit for the year of KShs. 126,408,000 (2006: Kshs.165,566,000) has been added to retained earnings. A final dividend for 2006 amounting to KShs. 126,000,000 was paid during the year (2006: Nil).

**DIRECTORS**

The present membership of the Board is set out on Page 13 and 14.

**AUDITORS**

The company's auditors, DCDM Associates were appointed during the year and express their willingness to continue in office in accordance with Section 159(2) of the Companies Act.

**By order of the Board**

**Issa Timamy**
**Company Secretary**

______________________________**2008**

**EVEREADY EAST AFRICA LTD**

**STATEMENT OF DIRECTORS' RESPONSIBILITIES**
**FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2007**

The Companies Act requires the Directors to prepare financial statements for each financial year that give a true and fair view of the state of affairs of the Company as at the end of the financial year and of its profit or loss. It also requires the Directors to ensure that the Company keeps proper accounting records that disclose, with reasonable accuracy, the financial position of the Company. They are also responsible for safeguarding the assets of the Company.

The Directors accept responsibility for the annual financial statements, which have been prepared using appropriate accounting policies supported by reasonable and prudent judgements and estimates, in conformity with International Financial Reporting Standards and the requirements of the Companies Act. The Directors are of the opinion that the financial statements give a true and fair view of the state of the financial affairs of the Company and of its profit or loss. The Directors further accept responsibility for the maintenance of accounting records that may be relied upon in the preparation of financial statements, as well as adequate systems of internal financial control.

Nothing has come to the attention of the Directors to indicate that the Company will not remain a going concern for at least twelve months from the date of this statement.

**Director** : ______________________________

**Director** : ______________________________

**Date** : ______________________________

## INDEPENDENT AUDITORS' REPORT TO THE MEMBERS FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2007

This report is made solely to the members of Eveready East Africa Limited (the "Company"), as a body, in accordance with Section 159 of the Companies Act (CAP 486). Our audit work has been undertaken so that we might state to the Company's members those matters we are required to state to them in an auditor's report and for no other purpose. To the fullest extent permitted by law, we do not accept or assume responsibility to anyone other than the Company and the Company's members as a body, for our audit work, for this report, or for the opinions we have formed.

### REPORT ON THE FINANCIAL STATEMENTS

We have audited the financial statements of Eveready East Africa Limited set out on pages 20 to 39 which comprise the balance sheet at September 30, 2007, and the income statement, statement of changes in equity and cash flow statement for the year then ended, and a summary of significant accounting policies and other explanatory notes.

**1. Directors' Responsibility for the Financial Statements**

The Directors are responsible for the preparation and fair presentation of these financial statements in accordance with International Financial Reporting Standards and in compliance with the requirements of the Kenyan Companies Act. This responsibility includes: designing, implementing and maintaining internal controls relevant to the preparation and fair presentation of financial statements that are free from material misstatement whether due to fraud or error; selecting and applying appropriate accounting policies; and making accounting estimates that are reasonable in the circumstances.

**2. Auditors' Responsibility**

Our responsibility is to express an opinion on these financial statements based on our audit. We conducted our audit in accordance with International Standards on Auditing. Those Standards require that we comply with ethical requirements and plan and perform the audit to obtain reasonable assurance whether the financial statements are free from material misstatement.

An audit involves performing procedures to obtain audit evidence about the amounts and disclosures in the financial statements. The procedures selected depend on the auditors' judgement, including the assessment of the risks of material misstatement of the financial statements, whether due to fraud or error. In making those risk assessments, the auditors consider internal control relevant to the Company's preparation and fair presentation of the financial statements in order to design audit procedures that are appropriate in the circumstances, but not for the purpose of expressing an opinion on the effectiveness of the Company's internal control. An audit also includes evaluating the appropriateness of accounting policies used and the reasonableness of accounting estimates made by the directors, as well as evaluating the overall presentation of the financial statements.

We believe that the audit evidence we have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for our audit opinion.

**3. Opinion**

In our opinion, the financial statements on pages 20 to 39 give a true and fair view of the financial position of the Company at September 30, 2007, and of its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Financial Reporting Standards and comply with the Kenyan Companies Act.

**4. Report on Other Legal and Regulatory Requirements**

As required by the Kenyan Companies Act we report to you, based on our audit, that:

i) we have obtained all the information and explanations which to the best of our knowledge and belief were necessary for the purposes of our audit;
ii) in our opinion proper books of account have been kept by the Company, so far as appears from our examination of those books; and
iii) the financial statements of the Company are in agreement with the books of account.

**Certified Public Accountants**
**Nairobi, Kenya**

**………………………….. 2007**

**EVEREADY EAST AFRICA LTD**

**INCOME STATEMENT**
**FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2007**

| | Notes | 2007 KShs'000 | 2006 KShs'000 |
|---|---|---|---|
| **Sales** | | **2,232,143** | 2,029,462 |
| Cost of sales | | **(1,669,303)** | (1,460,073) |
| **Gross profit** | | **562,840** | 569,389 |
| Other operating income | | **8,285** | 23,266 |
| Selling expenses | | **(94,822)** | (104,346) |
| Other expenses | | **(288,323)** | (236,452) |
| **Operating profit** | 6 | **187,980** | 251,857 |
| Finance costs | 8 | **(8,475)** | (17,821) |
| **Profit before income tax** | | **179,505** | 234,036 |
| Income tax expense | 9 | **(53,097)** | (68,470) |
| **Profit for the year** | | **126,408** | 165,566 |

**Earnings per Share attributable to the equity holders of the company (KShs. per share)**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Basic | 10 | **0.602** | 788 |
| Diluted | 10 | **0.602** | 0.788 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Dividends:** | | | |
| Interim dividend paid | 11 | - | - |
| Final dividend proposed | 11 | **94,500** | 126,000 |
| | | **94,500** | 126,000 |

**EVEREADY EAST AFRICA LTD**

**BALANCE SHEET**
**AS AT 30 SEPTEMBER 2007**

| | Notes | 2007 KShs'000 | 2006 KShs'000 |
|---|---|---|---|
| **CAPITAL EMPLOYED** | | | |
| Share capital | 12 | **210,000** | 210,000 |
| Retained earnings | | **138,585** | 106,677 |
| Proposed dividends | 11 | **94,500** | 126,000 |
| **Shareholders' funds** | | **443,085** | 442,677 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Provision for liabilities and charges | 22 | **92,900** | 82,900 |
| Hire purchase liabilities | 13 | **8,857** | - |
| | | **101,757** | 82,900 |
| | | **544,842** | 525,577 |
| **REPRESENTED BY** | | | |
| **Non-current assets** | | | |
| Property, plant and equipment | 16 | **162,234** | 139,248 |
| Prepaid operating lease rentals | 17 | **223** | 227 |
| Deferred tax | 14 | **15,438** | 24,372 |
| Retirement benefit asset | 15 | **6,143** | 11,621 |
| | | **184,038** | 175,468 |
| **Current assets** | | | |
| Inventories | 18 | **793,647** | 500,758 |
| Receivables | 19 | **174,769** | 163,434 |
| Current income tax receivable | | **21,974** | 1,050 |
| Cash and bank balances | 20 | **14,889** | 78,296 |
| | | **1,005,279** | 743,538 |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables and accrued expenses | 21 | **228,165** | 201,666 |
| Borrowings | 13 | **411,970** | 191,763 |
| Hire purchase liabilities | 13 | **4,340** | - |
| | | **644,475** | 393,429 |
| **Net current assets** | | **360,804** | 350,109 |
| | | **544,842** | 525,577 |

The financial statements on pages 20 to 39 were approved for issue by the board of Directors on 23/1/ 2008 and signed on its behalf by:

**Director** ________________ **Director** ________________

EVEREADY EAST AFRICA LTD

## STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY
## FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2007

| | Notes | Share capital KShs'000 | Retained earnings KShs'000 | Dividends KShs'000 | Total KShs'000 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Year ended 30 September 2006** | | | | | |
| At start of period | | 210,000 | 67,111 | - | 277,111 |
| Profit for the period | | - | 165,566 | - | 165,566 |
| Dividend proposed | 11 | - | (126,000) | 126,000 | - |
| Dividends paid in the year | 11 | - | - | - | - |
| **At end of year** | | **210,000** | **106,677** | **126,000** | **442,677** |
| **Year ended 30 September 2007** | | | | | |
| At start of period | | 210,000 | 106,677 | 126,000 | 442,677 |
| Profit for the period | | - | 126,408 | - | 126,408 |
| Dividend proposed | 11 | - | (94,500) | 94,500 | - |
| Dividends paid in the year | 11 | - | - | (126,000) | (126,000) |
| **At end of year** | | **210,000** | **138,585** | **94,500** | **443,085** |

**EVEREADY EAST AFRICA LTD**

**CASH FLOW STATEMENT**
**FOR THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2007**

| | Notes | 2007<br>K Shs'000 | 2006<br>K Shs'000 |
|---|---|---|---|
| **Operating activities** | | | |
| Cash generated from operations | 25 | **(37,334)** | 288,311 |
| Interest received | | **138** | 72 |
| Interest paid | | **(30,020)** | (23,313) |
| Income tax paid | | **(65,086)** | (69,616) |
| Net cash generated from operating activities | | **(132,302)** | 195,454 |
| **Investing activities** | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | 16 | **(45,478)** | (71,852) |
| Proceeds from disposal of property, plant and equipment | | **6,969** | 26,630 |
| Net cash used in investing activities | | **(38,509)** | (45,222) |
| **Financing activities** | | | |
| Proceeds from borrowings | | **14,047** | - |
| Repayments of borrowings | | **(850)** | - |
| Dividends paid | | **(126,000)** | - |
| Net cash used in financing activities | | **(112,803)** | - |
| **(Decrease)/increase in cash and cash equivalents** | | **(283,614)** | 150,232 |
| **Movement in cash and cash equivalents** | | | |
| At start of year | | **(113,467)** | (263,699) |
| (Decrease)/increase | | **(283,614)** | 150,232 |
| At end of year | 20 | **(397,081)** | (113,467) |

**1 General information**

Eveready East Africa Limited is incorporated in Kenya under the Companies Act and is domiciled in Kenya. The financial statements were authorised for issue by the board of directors on 23rd January, 2008

**2 Summary of significant accounting policies**

